

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA


(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)

MKOA WA SIMIYU

Simu: 0282 – 981193

Fax : 0282 - 981194

Email : dedbusegadc.go.tz



Sanduku la Posta 157

BUSEGA

Kumb. Na.BDC/C.30/17/50

06 Novemba, 2019

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilayaya Busega kwa kushirikiana na AGPAHI anawatangazia nafasi za ajira kwa mkataba wa mwaka mmoja katika vituo vya kutolea huduma na tiba. Hivyo basi watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi zilizoainishwa hapo chini watume maombi.

1. MSAIDIZI WA HESABU (nafasi 1) TGS B1

(a) Sifa za kuajiriwa

Kuajiriwa wenye cheti cha ATEC level 11 au “foundation level” kinachotolewa na NBAA, waombaji wawe na uzoefu wa kazi Zaidi ya mwaka (1) katika fani hiyo.

(b) Kazi na majukumu

- (i) Kuandika na kutunza “register” zinazohusu shughuli za uhasibu
- (ii) Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha
- (iii) Kutunza majalada yenye kumbukumbu za hesabu
- (iv) Kupeleka barua/yaraka za uhasibu benki
- (v) Kufanya usuluhisho wa masurufu, karadha , Hesabu za Benki na Amana.

2. DATA CLERK (nafasi 1) TGS B1

(a) Sifa za kuajiriwa

Kuajiriwa wenye astashahada ya IT, takwimu au utunzaji wa kumbukumbu kwa njia ya kielektroniki awe na uzoefu wa takwimu za afya (health Data experience) awe na uzoefu wa kutumia mfumo wa DHIS, EXCEL,MS, ACCESS, PEINFO, SSP na uzoefu wa mifumo mingine itakuwa sifa ya ziada .

(b) Kazi na majukumu

- (i) Utunzaji wa mfumo wa CTC, data base
- (ii) Kuhuisha CTC data base
- (iii) Kuingiza takwimu za wagonjwa kila siku na kutengeneza taarifa na kuwasilisha katika ngazi husika
- (iv) Kurudisha faili za wagonjwa ambao hazijajazwa kwa mganga (clinical zirekebishwe)
- (v) Kuhakikisha kila file la mgonjwa linakuwa na fomu ya kuchunguza ugonjwa wa kifua kikuu na magonjwa ya STI na kuhakikisha zinajazwa na mganga kila mgonjwa anapohudhuria kliniki.
- (vi) Kutengeneza mpango kazi wa kuboresha takwimu katika kituo husika katika mfumo wa CTC, Data base na katika vyanzo vya takwimu.
- (vii) Kuhakikisha matumizi sahihi ya mafumo unafanya kazi kila siku, kila wakati kuhusisha nati virus kila siku
- (viii) Kuhakikisha unawasiliana na viongozi wako kwa wakati kwa ajili ya kukarabati mfumo pindi tatizo linapotokea
- (ix) Kuingiza data CTC2 waishio na VVU/ukimwi kwenye komputa
- (x) Kusafisha data husika kila mara kaitika data ya mradi
- (xi) Kuandaa ripoti za kila mwezi na kuwasilisha kwa msimamizi wake wa kazi

Pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na mwajiri.

MASHARTI YA UJUMLA KWA WAOMBAJI

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
2. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
3. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi CV, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waloifika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.
4. Picha moja passport size iandikwe jina kwa nyuma
5. Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (statement of Result havitakubalika)
6. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kingereza au Kiswahili na yatumwe kwa njia ya Posta kabla ya tarehe 14/11/2019 kwa anwani ifuatayo.

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya wilaya
S.L.P 157,
BUSEGA.



Anderson N. Kabuko
Mkurugenzi Mtendaji

Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
BUSEGA DISTRICT COUNCIL
BUSEGA